



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA**



*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb.Na. TMC/U/193 VOL. IV/19**

**Tarehe: 10.07.2021**

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Kwa mujibu wa Kibali cha ajira mbadala kilichotolewa na Katibu Mkuu (Utumishi) kupitia barua yenye Kumb. Na. FA.170/365/01"B"/117 ya tarehe 16 Juni, 2021 Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora anawatangazia nafasi za kazi wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi hizo kama ifuatavyo:-

### **1. MTENDAJI WA MTAA III – NAFASI 2**

#### **SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe na elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu Mafunzo ya Astashahada (Certificate) katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **KAZI NA MAJUKUMU**

- i. Katibu wa Kamati ya Mtaa na Mtendaji Mkuu wa Mtaa
- ii. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya maendeleo katika Mtaa
- iii. Msimamizi wa Utekelezaji wa Sera na Sheria ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa.
- iv. Msimamizi na mshauri Mkuu kuhusu masuala ya ulinzi na usalama katika Mtaa.
- v. Kusimamia mapato na matumizi katika Mtaa
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika Mtaa wake na kuhamasisha wananchi kuandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa.

**MSHAHARA** – Kwa kuzingatia ngazi ya mshahara wa Serikali yaani **TGS B**

## **MASHARTI YA JUMLA**

- ✓ Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 hadi 45 na lazima awe raia wa Tanzania.
- ✓ Mwombaji wa ajira analazimika kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- ✓ Maombi yaambatishwe na nakala za vyeti vya taaluma na mafunzo vilivyothibitishwa- result slip hazikubaliki, Cheti cha Kuzaliwa, maelezo binafsi (Curriculum Vitae) picha ndogo za rangi (Colored passport size) mbili (2)
- ✓ Mwombaji awe hajawahi kupatikana na hatia ya kosa la jinai na kufungwa jela
- ✓ Waombaji wenye sifa pungufu au zaidi ya zilizotajwa hapo juu hawashauriwi kuomba.

## **JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote za maombi zitumwe zikiwa na anwani kamili ya mwombaji pamoja na namba ya simu kwa anwani ifuatayo:-

**MKURUGENZI WA MANISPAA,  
HALMASHAURI YA MANISPAA,  
S.L.P. 174,  
TABORA**

**Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni 30.07.2021 saa 9.30  
alasiri**

Tangazo hili limetolewa na;



Bosco O. Ndunguru  
**MKURUGENZI WA MANISPAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA  
TABORA**